

Ni lazima wawe karantini (quarantine) au ujitenge kwasababu ya COVID-19, na hauna mda wa likizo wa malipo?

Programu ya Likizo Fupi ya Malipo (Temporary Paid Leave Program) ya COVID-19 husaidia wafanyikazi wanaohitaji wawe karantini au kujitenga kwasababu ya kukaribia COVID-19 au wanapohisi ishara zake na wanahitaji ushauri wa kimatibabu, lakini hawastahili likizo ya ugonjwa yenye malipo inayohusiana na COVID-19 (au hawana namna ya kupata mda wa likizo ya malipo inayohusiana na COVID-19).

Watu wanaostahili watapokea malipo ya \$120 kila siku kwa mda usiozidi siku 10 za kazi (\$1,200 jumla) kwa mda ambao wanahitaji wakarantini au kujitenga.

Wafanyikazi lazima watimize mahitaji yote yafwatayo ili wastahili mradi huu:

- Kufanya kazi Oregon na kutakiwa kujaza ushuru wa mapato wa Oregon.
- Wameshauriwa wakarantini na almashauri ya afya ya eneo au ya kabila au mhudumu wa afya kwasababu ya kukaribia mtu aliyeambukizwa au mwenye ishara zinazohusiana na COVID-19 na wanatafuta ushauri wa kimatibabu.
- Kutoweza kufanya kazi (pamoja na kazi akiwa nyumbani) kwasababu wanahitaji karantini au kujitenga.
- Hakupata mapato jumla yaliyosahihiswa (adjusted gross income) ya zaidi ya \$60,000 binafsi au \$120,000 pamoja kwenye ushuru wao wa Oregon wa 2019. Kama walichuma zaidi ya \$60,000 binafsi au \$120,000 pamoja mwaka 2019 au kama hawakujaza ushuru wa Oregon wa 2019, basi watastahili ikiwa hawatarajii kupokea hadi \$60,000 binafsi au \$120,000 pamoja mwaka 2020. MUHIMU: Mapato jumla yaliyosahihiswa kwenye ushuru binafsi wa Oregon wa mwaka 2019 uko laini ya 7 ya Form 40 (wenyeji wa mwaka mzima), na laini 29F ya Form 40N (wasiokuwa wenyeji) na 40P (wenyeji wa sehemu ya mwaka).
- Muajiri wao hapeani likizo ya malipo ya ugonjwa unaohusiana na COVID-19 ama wamemaliza likizo yao ya malipo iliyopo ya ugonjwa unaohusiana na COVID-19.
- Hawafanyi maombi ya marupurupu ya bima ya wasiokuwa na kazi (unemployment insurance) kwa mda hawatakuwa kazini kwasababu ya karantini au kujitenga.
- Hawafanyi maombi ya marupurupu ya wafanyikazi kwa mda hawatakuwa kazini kwasababu ya karantini au kujitenga au wakihisi ishara za COVID-19.
- Hawatafuti au hawatumii marupurupu kutokana na programu kama hizi za usadizi wa karantini ya COVID-19 katika Oregon au jimbo jengine.
- Hawafanyi maombi au hawapokei aina nyengine za likizo ya malipo kutoka kwa muajiri wao wakati wa karantini yao au wanapojitenga, kama vile hifadhi ya likizo ya ugonjwa au likizo ya mwaka.
- Hawakufutwa au kusimamishwa kazi na muajiri wao.
- Lazima wawe wamemjulisha muajiri wao kuwa wanahitaji karantini au kujitenga.
- Wanaweza kudai mda mmoja tu wa karantini.

Wafanyikazi wanaostahili lazima wajaze fomu ya mtandao katika oregon.gov/covidpaidleave na wataombwa wapeane maelezo binafsi, maelezo ya muajiri na ya kampuni, na maelezo ya karantini. Kama hauna namna ya kufanya maombi kwa mtandao, piga 833-685-0850 (bila malipo) au 503-947-0130. Kwa usaidizi kwa lugha nyengine, piga 503-947-0131. Kwa maelezo zaidi, tazama oregon.gov/covidpaidleave.

Kuambatana na Sheria ya Waamerika Wenye Kilema [Americans with Disabilities Act (ADA)], chapisho hili linapatikana kwa mifumo mingine. Piga 503-947-0130.